2011

Tazama: Naja—

upesi

Ufunuo 22:12

Januari/Janvier

J'pili	J'tatu	J'nne	J'tano	Alh.	Ijumaa	J'mosi
30	31					1
2	3	4	5	6	7	8
9	10	11	12	13	14	15
16	17	18	19	20	21	22
23	24	25	26	27	28	29

Februari/Février

J'pili	J'tatu	J'nne	J'tano	Alh.	Ijumaa	J'mosi
		1	2	3	4	5
6	7	8	9	10	11	12
13	14	15	16	17	18	19
20	21	22	23	24	25	26
27	28					

Machi/Mars

J'pili	J'tatu	J'nne	J'tano	Alh.	Ijumaa	J'mosi
		1	2	3	4	5
6	7	8	9	10	11	12
13	14	15	16	17	18	19
20	21	22	23	24	25	26
27	28	29	30	31		

Aprili/Avril

J'pili	J'tatu	J'nne	J'tano	Alh.	Ijumaa	J'mosi
					1	2
3	4	5	6	7	8	9
10	11	12	13	14	15	16
17	18	19	20	21	22	23
24	25	26	27	28	29	30

Mei/Mai

J'pili	J'tatu	J'nne	J'tano	Alh.	Ijumaa	J'mosi
1	2	3	4	5	6	7
8	9	10	11	12	13	14
15	16	17	18	19	20	21
22	23	24	25	26	27	28
29	30	31				

Juni/Juin

J'pili	J'tatu	J'nne	J'tano	Alh.	Ijumaa	J'mosi
			1	2	3	4
5	6	7	8	9	10	11
12	13	14	15	16	17	18
19	20	21	22	23	24	25
26	27	28	29	30		

Julai/Juillet

J'pili	J'tatu	J'nne	J'tano	Alh.	Ijumaa	J'mosi
31					1	2
3	4	5	6	7	8	9
10	11	12	13	14	15	16
17	18	19	20	21	22	23
24	25	26	27	28	29	30

Agosti/Août

J'pili	J'tatu	J'nne	J'tano	Alh.	Ijumaa	J'mosi
	1	2	3	4	5	6
7	8	9	10	11	12	13
14	15	16	17	18	19	20
21	22	23	24	25	26	27
28	29	30	31			

Septemba/Septembre

J'pili	J'tatu	J'nne	J'tano	Alh.	Ijumaa	J'mosi
				1	2	3
4	5	6	7	8	9	10
11	12	13	14	15	16	17
18	19	20	21	22	23	24
25	26	27	28	29	30	

Oktoba/Octobre

J'pili	J'tatu	J'nne	J'tano	Alh.	Ijumaa	J'mosi
30	31					1
2	3	4	5	6	7	8
9	10	11	12	13	14	15
16	17	18	19	20	21	22
23	24	25	26	27	28	29

Novemba/Novembre

J'pili	J'tatu	J'nne	J'tano	Alh.	Ijumaa	J'mosi
		1	2	3	4	5
6	7	8	9	10	11	12
13	14	15	16	17	18	19
20	21	22	23	24	25	26
27	28	29	30			

Desemba/Décembre

J'pili	J'tatu	J'nne	J'tano	Alh.	Ijumaa	J'mosi
				1	2	3
4	5	6	7	8	9	10
11	12	13	14	15	16	17
18	19	20	21	22	23	24
25	26	27	28	29	30	31

"Mtafuteni BWANA, maadamu anapatikana, mwiteni, maadamu yu karibu; mtu mbaya na aache njia yake, na mtu asiye haki aache mawazo yake; na amrudie BWANA, naye atamrehemu; na arejee kwa Mungu wetu, naye atamsamehe kabisa."

Isaya 55:6, 7

"Roho ya Bwana MUNGU i juu yangu; kwa sababu BWANA amenitia mafuta niwahurbiri wanyenyekevu habari njema; amenituma ili kuwaganga waliovunjika moyo, kuwatangazia mateka uhuru wao, na hao waliofungwa habari za kufunguliwa kwao. Kutangaza mwaka wa BWANA uliokubaliwa, na siku ya kisasi cha Mungu wetu; kuwafariji wote waliao; kuwaagizia hao waliao katika Sayuni, wapewe taji ya maua badala ya majivu, mafuta ya furaha badala ya maombolezo, vazi la sifa badala ya roho nzito; wapate kuitwa miti ya haki, iliyopandwa na BWANA, ili atukuzwe."

Isaya 61:1-3

"Tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru."
"Basi Mwana akiwaweka huru, mtakuwa huru kweli kweli."

Yohana 8:32, 36

Kata hapa

Jina..... Umri: .....

Anwani.....

.....

Nchi.....

Andika e-mail yako hapa, ukiwa nayo: .....

117

- UKITAKA KUPOKEA NAKALA YA UPESI BILA MALIPO, jaza na ututumie cheti hiki nasi tutakutumia bure nakala ya *UPESI* kwa mwaka.
- **Andika jina na anwani yako kwa HERUFI KUBWA. Kisha tuma kwa: *UPESI*, Willington, Derby, England, DE65 6BN**
- Ukituma barua bila stampu, au ukitumia stampu zisizo mpya, barua haitatufikia.
- Ukitaka kusoma *UPESI* kwenye INTERNET, tumia: soon.org.uk/swahili
- Ili kupokea magazeti ya *UPESI* kwa njia ya posta tafadhali andika na kutuma anwani yako kwa: upesi-office@soon.org.uk
- Ili kupokea gazeti la *UPESI* kwa njia ya email, tafadhali tuma email isiyoandikwa chochote kwa hii awani, upesi-subscribe@soon.org

ISSN 1472-7285

Alikufa ili kuokoa wengine

sxc.hu

Mlinzi mmoja wa mlango aliokoa maisha ya wanawake wengi katika Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Pakistan. Mnamo tarehe 20 Oktoba 2009 kuna mtu alijaribu kuua wanafunzi wengi kwa kuwashambulia kwa bomu. Wasichana watatu waliuawa siku ile, lakini hali ingalikuwa mbaya zaidi kama mlinzi wa mlango aitwaye Pervaiz Masih, ambaye naye aliuawa, asingalionyesha ujasiri mwingi.

Alimzuia mshambuliaji

"Kama asingalimzuia yule mshambuliaji, watu wengi zaidi wangalikuwa wameuawa," ndivyo alivyosema mmoja wa wanafunzi. "*Watu watamkumbuka yeye pamoja na alilolifanya."* Masih alimzuia mshambuliaji mlangoni na lile bomu likaangukia nje ya jengo ambalo lilikuwa na wanawake wengi ndani. *"Vipande vingi vya vyuma vilivyotoka katika bomu lile viliangukia kwenye sehemu ya kuegesha magari badala ya kwenda kwenye ukumbi ambako kulikuwa na wasichana kati ya 300 na 400 waliokuwa wamekaa,"* ndivyo alivyoeleza Profesa Fateh Muhammad Malik, ambaye ni Mkuu wa Chuo Kikuu hicho. *"Pervaiz Masih hakuacha mawazo mbalimbali ya dini yamzuie kutenda lililo jema. Ingawa alikuwa ni Mkristo aliyetoa maisha yake kwa ajili ya wasichana Waislamu."*

Masih alikuwa ni mmoja wa Jamii ndogo ya Kikristo ya Pakistan. Wakristo ni moja ya makundi maskini sana katika nchi ile. Mshambuliaji alipokuja, Masih alikuwa amefanya kazi kwa siku zisizofikia wiki moja kwa mshahara mdogo sana. Masih aliishi na watu wengine saba katika familia ndani ya chumba kimoja kilichojaa sana kwenye jiji kubwa.

Pervaiz Masih alikufa ili kuwaokoa wanafunzi wasife. Hili linatukumbusha jinsi Yesu Kristo alivyokufa kutuokoa na dhambi zetu na kutupa uzima.

Nilijifunza kutumia bunduki

Tom ni msomaji wa *UPESI* aliyeko gerezani nchini Nigeria

Nikiwa na umri wa miaka 13 nilienda kuishi na mjomba wangu ambaye alinipeleka shule. Nilifanya vizuri sana shuleni lakini pia kule shuleni nilikutana na wavulana kadhaa ambao walinifundisha kuiba. Wao walikuwa ni wakubwa kwa umri kunizidi. Kwa hiyo nilifanya kila kitu walichoniagiza, hata kama nilijua kuwa kile nilichokuwa nikikifanya kilikuwa kibaya.

Mjomba aligundua

sxc.hu

Kila niliporudi nyumbani kutoka shuleni niliingia chumbani kwa mjomba na kumwibia fedha kutoka mfukoni mwake. Kisha nilienda kutumia hizo fedha pamoja na hao wavulana kwenye vikundi vya starehe. Mara mjomba alifahamu nilichokuwa nikikifanya na akaniambia, *"Acha tabia hii maana hatuishi namna hii!"* Lakini kweli sikumsikiliza alichokuwa akiniambia na badala yake nilitoroka nyumbani kwake.

Maisha yangu yakazidi kuwa mabaya. Nikaanza kuwaibia watu nyumbani kwao na kuanza kutumia madawa ya kulevya.

Nilijifunza hata kutumia bunduki. Maovu yangu yalikithiri na yalitishia amani. Nikiwa na umri wa miaka 15, tayari nilikuwa jambazi!

Nilifungwa jela

Nilipofikia umri wa miaka 20, nilikamatwa na polisi na kupelekwa mahakamani. Hakimu alinihukumu na akasema, *"Lazima uende jela miaka mitatu."*

Nikiwa gerezani, Wakristo fulani walifika kule kutuambia habari za Yesu Kristo. Kila neno walilolisema lilinifanya nitafakari maisha yangu na mambo ambayo nilikuwa nimeyafanya.

Baadhi ya marafiki niliowakuta kule gerezani walikuwa pia ni wafuasi wa Yesu Kristo. Waliniambia kuwa ningeweza kumjua Mungu na kujua jinsi Yesu alivyokuja duniani, akafa ili mimi nisamehewe. Nilitambua kuwa Yesu alikufa kwa ajili ya kuchukua adhabu ambayo ni mimi niliistahili kutokana na dhambi nilizozifanya.

Nilipojifunza mambo haya nilianza kujisikia tofauti. Nilimwomba Mungu anisamehe. Lilikuwa ni jambo la ajabu mno ambalo liliwahi kunitokea. Sasa nimekuwa huru moyoni. Sasa ninawafundisha wengine yale mambo niliyojifunza gerezani.

Sikiliza Redio!

Sikiliza Habari Njema katika lugha ya Kiswahili:

Redio Habari Maalum: 11885 kHz, Metabendi 25, kila siku

TWR: 9475Khz MB 31, 1700-1800 UTC
6110Khz MB49, 0300-0330 UTC

IBRA: 9520Khz MB31, 1730-1830 UTC

Mombasa-Baraka FM – Kwenye 95.5FM katika Kiswahili na Kiingereza
Na kwenye vipindi vya **FM** nyingi
Ukipenda kuona nyingine, tazama: soon.org.uk/radio

Jifunza kitabu cha Mungu

Ukitaka kupata Masomo ya Biblia katika lugha ya Kiswahili kwa posta, tuma jina na anwani yako kwa:

Katika KENYA: Emmaus Shule ya Biblia, SLP 72725, Nairobi, Kenya

Katika CONGO: Cours Biblique Emmaus, BP 350 Bunia, Rég. du Haut-Congo, Rép. Dém. du Congo

Katika TANZANIA: Emmaus Shule ya Biblia, SLP 1424 Dodoma, Tanzania. Wanasubiri barua yako ili uweze kutumiwa somo lako la kwanza bila malipo.

Basi liligonga ukuta

Neema kutoka Ghana anajua kuwa Mungu aliokoa maisha yake

Paul Little

Nilikuwa naelekea nyumbani jioni moja wakati nilipoona basi likiendeshwa kwa uzembe. Lilikuwa linapita kila upande wa barabara. Ghafla, lilielekea kwangu. Sikuwa na muda wa kukwepa. Nilijua kuwa basi hilo lingenigonga na ningekufa.

Dakika chache baadaye nilidhani tayari niko mbinguni, lakini niligundua kumbe bado nilikuwa hai. Nilikuwa nimelala kwenye mtaro mkavu pembeni mwa barabara. Watu waliniambia kuwa basi lilikuja mahali nilipokuwa nikitembea na kupita juu ya mtaro. Likaishia kugonga ukuta wa nyumba.

Sikujua cha kufanya. Sikuweza kusimama mwenyewe. Kisha mtu mmoja niliyemfahamu, alikuja. Alikuwa ni Kofi akielekea nyumbani na rafiki yake. Kwa pamoja walinishika mikono na kunipeleka hospitali. Nilivunjika mfupa wa mguuni – halikuwa na tatizo jingine lolote, na wala sikuwa na maumivu makali kwenye mguu wangu. Mungu alifanya jambo la ajabu kwangu siku hiyo. Aliniokoa na kifo. Sitaweza kufahamu ni kwa vipi basi halikuniua. Sasa hivi ni mzima na ninamshukuru Mungu kwa kuokoa maisha yangu.

Tunaweza kuwa huru!

Jacques ni mfuasi wa Yesu anayeishi Benin, Afrika Magharibi

Asubuhi moja niliamka na maumivu makali upande wa juu wa mguu wangu. Hata hivyo sikuwaza kuhusa yake tena siku hiyo. Asubuhi iliyofuata, niliyasikia tena maumivu hayo. Yalikuwa makali zaidi. Kulikuwa na uvimbe wenye usaha. Ulikuwa na hali mbaya kiasi kwamba nilianza kumeza vidonge ili kuondoa maumivu. Wazazi wangu waliniambia niende hospitali ili kikapasuliwe usaha utoke; lakini mimi sipendi hospitali. Nilisema, *"Hapana. Sitaenda hospitali, lakini nitamwomba Mungu aniponye."* Wazazi wangu nao waliomba kadhalika.

Maumivu yaliondoka

Kadiri siku zilivyoenda, niligundua kuwa uvimbe ulizidi kuwa na hali mbaya. Wazazi wangu waliingiwa na hofu, maana hawakupenda kuniona nikiteseka. Kisha wiki moja baadaye, uvimbe ule ulipasuka. Nikawekwa huru mbali na maumivu. Mungu alisikia maombi yangu na kuniponya bila hata ya msaada wa daktari wa hospitalini. Kadiri nilivyowaza kile kilichonitokea, nikagundua kuwa matatizo yetu yanaweza kuwa kama uvimbe. Nilipokuwa na uvimbe, nilikuwa nateseka na nilitembea kwa maumivu makali. Baada ya uvimbe huo kupasuka, nilikuwa huru kutembea kwa kawaida tena.

Tunapokuwa na tatizo maishani mwetu, tunaumia kwa ndani. Lakini tunaweza kumwomba Mungu atusaidie. Kadiri tatizo linavyokuwa kubwa, ndivyo tunavyotakiwa kuzungumza na Mungu na kuamini kuwa atatusaidia. Kisha Mungu atatuweka huru, kama ambavyo aliniweka huru dhidi ya maumivu yaliyosababishwa na uvimbe. Mungu ni msaidizi wetu katika kila tatizo maishani mwetu.